*Kioo cha Lugha, Juz. 23(1), 55-66*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DO: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v23i1.4

# Dhima ya Lugha ya Mhusika Mtoto katika Vichekesho Teule vya *Anko Zumo*

*Tuzo P. Bitesigirwe*[1] *na Edith B. Lyimo*[2]

## Ikisiri

Vichekesho ni kipera cha fasihi simulizi kinachoendelea kukua na kuendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia. Hii inamaanisha kuwa kama ambavyo mambo mengi yamebadilika kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia, sanaa ya vichekesho nayo imebadilika, hususani katika vipengele vya uhifadhi na uwasilishaji wake. Hivi sasa vichekesho vinawasilishwa kupitia mitandao mbalimbali ya kijamii, kama vile *YouTube*, *Instagram*, *Facebook* na *Twitter*. *Anko Zumo* ni miongoni mwa vichekesho vinavyowasilishwa kupitia mitandao ya kijamii. Vichekesho hivi hutumia wahusika watu wazima na watoto. Miongoni mwa wahusika wakuu wa vichekesho hivi ni mtoto Maisara Mohamed maarufu kama Mai Zumo. Mhusika huyu anatumia lugha ili kuivutia hadhira na kuifanya icheke. Licha ya kuivutia hadhira na kuifanya icheke, zipo tafiti mbalimbali zinazoonesha kuwa matumizi ya watoto katika kazi za sanaa hayafanyiki kiholela bali huwa na dhima anuwai. Suala hili liliibua makala hii ambayo imelenga kuchunguza dhima ya lugha ya mhusika mtoto katika vichekesho vya *Anko Zumo*. Data za makala hii zilipatikana kwa kuchunguza vichekesho teule tisa (9) kupitia mtandao wa *YouTube*. Uchambuzi wa data uliongozwa na Nadharia ya Uvunjaji wa Kanuni Usio na Madhara. Matokeo yanaonesha kuwa lugha ya mhusika mtoto katika vichekesho teule vya *Anko Zumo* ina dhima anuwai.

## 1.0 Utangulizi

Vichekesho ni sanaa inayokua kwa haraka. Maendeleo ya sayansi na teknolojia yaliyoimarika kuanzia karne ya ishirini na moja (21), yameleta mabadiliko makubwa katika tasnia hii ya vichekesho. Mathalani, Samwel (2013) na Mulokozi (2017) wanaeleza kuwa tofauti na ilivyokuwa kabla ya Azimio la Arusha,

[1] Mhadhiri Msaidizi, Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dodoma, Tanzania. Baruapepe: tuzop@rocketmail.com

[2] Mhadhiri Mwandamizi, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania. Baruapepe: edithbalyimo@gmail.com

kumeibuka mkondo mpya wa uwasilishaji wa vichekesho unaofanywa na baadhi ya vikundi kama *Vioja Mahakamani* na *Ze Orijino Komedi* kupitia televisheni. Sanjari na maendeleo haya, mitandao ya kijamii imekuwa mstari wa mbele katika kueneza vichekesho ambavyo huwafikia wanajamii kupitia simu zao za viganjani maarufu kama simu janja. Baadhi ya vichekesho vinavyopatikana katika mitandao ya kijamii ni kama vile vichekesho vya *Anko Zumo*, *Lucas Mhuvile* (Joti), na *Kansiime Anne*. Akichunguza suala la utendaji katika vichekesho vya *Ze Orijino Komedi*, Mwakisyala (2020) anafafanua kuwa wahusika katika vichekesho hivyo hutumia lugha, maleba, matendo na miondoko ili kuvutia hadhira na kuifanya icheke. Kutokana na maelezo hayo, hadhira ya vichekesho huvutiwa na kucheka kutokana na vionjo anuwai vilivyo katika lugha, maleba, miondoko na matendo ya wahusika. Wahusika katika vichekesho wanaweza kuwa watu wazima na watoto. Kwa upande wa watoto, Orellana (2017) anafafanua kuwa watoto hufurahisha sana kuliko watu wazima kwani katika vichekesho vyao huingiza pia masuala yanayogusa jamii nzima. Kwa kuthibitisha hoja yake, Orellana anaeleza kuwa hata watu wazima wanaofanya vichekesho, hufurahisha zaidi na kuvutia wanapoigiza lugha na matendo ya kitoto. Orellana anaongeza kuwa kwa asili watoto huvutia na hawachoshi. Kutokana na hali hii, watoto wanapoonekana katikati ya watu wazima hupewa kipaumbele na aghalabu watu wazima huvuta umakini katika kuwaangalia. Miongoni mwa mambo mengi ambayo watu wazima huvutiwa nayo ni lugha ya watoto. Wataalamu wanadokeza kuwa mara nyingi, lugha ya mhusika mtoto[3] huvuta hadhira kutokana na upekee wake kwa kulinganisha na lugha ya watu wazima (Wilkie na Saxton, 2010). Lugha hii hujengwa kwa kuzingatia umri wa mtoto, kiwango chake cha uelewa, mazingira anayokulia, nafasi yake katika jamii, na hulka ya watoto kwa ujumla (Kahigi, 1995). Kwa kawaida, lugha ya mtoto huwa na sifa ya kutumia sentensi fupi, msamiati rahisi, kuuliza maswali ya udadisi, kueleza hisia moja kwa moja bila kuficha, kutumia takriri pamoja na kutumia maneno ya kubuni au ya michezo (Kahigi, 1995; Wilkie na Saxton, 2010; Ngugi, 2018).

Katika muktadha huu wa vichekesho, lugha ya mhusika mtoto hupewa uzito wa kipekee kwa kuwa ndicho chombo kinachomwezesha mtoto huyo kufanikisha jukumu lake la kuibua kicheko. Mtoto anaweza kutumia lugha kwa njia isiyotarajiwa, kwa mfano, kusema ukweli wa wazi ambao watu wazima husita kuusema, kutumia kauli zenye mantiki ya kitoto lakini zinazofunua hali halisi ya jamii, au kuiga kauli za watu wazima kwa namna ya kuchekesha (Olajimbiti, 2018). Aidha, makosa ya kimatamshi au kimantiki yanayojitokeza katika usemi wa

[3] Katika makala hii, mtoto anayerejelewa yuko katika kundi la umri wa miaka mitatu hadi sita (Piaget, 1954; Bisht, 2008). Mtoto katika kundi hili huwa na kiwango kidogo cha msamiati, uelewaji na uundaji wa mantiki kwa kutumia lugha anayozungumza na anayosikia tofauti na watoto wenye umri wa juu.

mtoto huweza pia kuchukuliwa kuwa sehemu ya mbinu ya ucheshi katika vichekesho (Saxton, 2009).

Vichekesho vya *Anko Zumo* ni miongoni mwa kazi za sanaa nchini Tanzania zilizopata umaarufu mwishoni mwa mwaka 2016. Kati ya wahusika wa vichekesho hivi ni mtoto Maisara Mohamed maarufu kama Mai Zumo (Ernest, 2020). Vichekesho hivyo, maarufu kama *Anko Zumo* vinawasilishwa kwa muundo wa video fupi ambazo zimehifadhiwa katika mitandao ya kijamii ya *YouTube* na *Instagram*. Mara nyingi, Maisara amekuwa mhusika mkuu katika vichekesho hivyo. Pamoja naye, Maisara anaigiza na baba yake aitwaye Mohamed Omari (Anko Zumo) na wakati mwingine na mama yake aitwaye Habiba Zumo. Wahusika wengine ambao wanaigiza na Mai Zumo ni Omari Mohamed (kaka yake) na Mwanahamis Mfaume (shangazi yake). Vichekesho hivi vina watazamaji zaidi ya milioni mbili (2) katika mitandao ya *YouTube* na *Instagram* na hivyo kuonesha kuwa vinapendwa sana na hadhira. Kupendwa huko kunatokana na uwezo wa kutumia lugha alionao mhusika mtoto ili kuvutia hadhira na kuifanya icheke (Ernest, 2020). Aidha, zipo tafiti zinazoonesha kuwa mbali na kufurahisha au kuchekesha hadhira, wasanii huwatumia watoto kuwasilisha ujumbe anuwai (Sifaksi, 1979; Orellana, 2017; Olajimbiti, 2018; Bitesigirwe, 2021). Hivyo basi, makala hii inachunguza dhima ya lugha anayoitumia mhusika mtoto katika vichekesho *vya Anko Zumo.*

## 2.0 Kiunzi cha Nadharia

Data za makala hii zilichambuliwa na kuwasilishwa kwa kuongozwa na Nadharia ya Uvunjaji wa Kanuni Usio na Madhara. Nadharia hii iliyoasisiwa na Peter McGraw na Caren Warren (2010) inaelezea jinsi watu wanavyocheka au kujisikia vizuri wanaposhuhudia ukiukaji wa kanuni ambazo hazina madhara makubwa au hatari ya moja kwa moja. Nadharia hii inasisitiza kuwa ucheshi unatokana na hali ambapo uvunjaji wa kanuni unaonekana kuwa wa kawaida na usio na madhara (McGraw na Wolff, 2012). Kwa mujibu wataalamu hawa, misingi mikuu ya nadharia hii imejikita katika kitendo cha uvunjaji wa kanuni, kutokuwa na madhara na muktadha wa utulivu. Kwa maneno mengine, katika uvunjaji wa kanuni, lazima kuwe na aina fulani ya kuvunja kanuni au matarajio. Hali hii inaweza kutokea katika uvunjaji wa maadili, kama vile uvaaji au kuingilia mazungumzo ya watu. Pia, uvunjanji huo lazima uonekane kuwa hauna madhara. Ikiwa uvunjaji ni mkubwa sana, hautakuwa kichekesho bali utasababisha athari nyingine hususani inayokera. Mwisho, mtazamaji lazima aone uvunjaji na kutokuwa kwake na madhara kwa wakati mmoja. Uwiano huu kwa pamoja unaleta kichekesho. Nadharia hii ilikuwa faafu katika kuchambua dhima ya lugha ya mhusika mtoto kwa sababu mara nyingi watoto huvunja sheria za mazungumzo hususani wanapotumia maneno yasiyo sahihi, kuchukua maneno kwa maana halisi

au kutokuelewa utani. Kutokana na hali yao ya utoto, uvunjaji huo huonekana kuwa hauna madhara, jambo linalosababisha vichekesho.

## 3.0 Mbinu za Utafiti

Data za makala hii zilikusanywa maktabani kwa kutazama vichekesho vya *Anko Zumo* vilivyohifadhiwa katika mtandao wa *YouTube.* Sampuli iliyotumika ilitokana na vichekesho 60 vya *Anko Zumo.* Mbinu ya usampulishaji lengwa ilitumiwa kupata vichekesho 27 vilivyomhusisha mhusika mtoto. Mbinu hii ilitumika kimakusudi kwa kuwa si vichekesho vyote vya *Anko Zumo* vilivyomhusisha mhusika mtoto. Hivyo, baada ya kupata vichekesho hivyo, tuliviandika majina yake na kuvipatia namba 1 hadi 27. Ili kupata sampuli kinasibu, tuliteua kwa kuruka namba 3. Kwa mantiki hii, vichekesho vilivyopatikana kwa mchakato huo vilichukuliwa kama sampuli. Usampulishaji nasibu ulifanikisha kupata vichekesho 9 vyenye mhusika mtoto ambapo lugha anayotumia ndiyo kichocheo cha makala hii. Ili kurahisisha zoezi la uchambuzi na uwasilishaji wa data, vichekesho teule vilitambuliwa kwa namba, yaani *Kichekesho Na. 1* hadi *Na. 9.* Data katika vichekesho hivyo zilikusanywa kwa njia ya utazamaji wa vichekesho. Vilevile, data hizo zilichanganuliwa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli.

## 4.0 Dhima za Lugha ya Mhusika Mtoto Katika Vichekesho Teule

Katika sehemu hii tumefafanua dhima za lugha ya mhusika mtoto katika vichekesho teule vya *Anko Zumo*. Dhima zilizobainika ni kuchochea udadisi, kuibua na kufanya hadhira itambue hisia za watoto, kuibua ucheshi, kufichua uovu, kukuza na kupamba lugha, na kuwasilisha tajiriba za watu wazima. Ufafanuzi wa dhima hizi unatolewa kama ifuatavyo:

### 4.1 Kuchochea Udadisi kwa Mtoto

Kudadisi ni kupeleleza jambo ili kujua undani wake. Mara nyingi udadisi huendana na maswali mbalimbali yanayomfanya mdadisi ajue ukweli wa jambo. Maswali hayo yanaweza kuwa ya kitashtiti, yaani kuuliza swali ambalo jibu lake linajulikana (Senkoro, 2011). Watoto ni kundi ambalo hupenda udadisi. Bruner (1983) anaeleza kwa asili watoto wanapenda kudadisi, hivyo, lugha hutumika kama nyenzo kuu ya kufanikisha udadisi wao. Hoja yake inasisitizwa na Ngugi (2014) anayeeleza kuwa mbali na mahitaji ya kimwili, watoto huwa na hitaji la kudadisi na kutekeleza udadisi huo. Hii inaonesha kuwa watoto hutaka kudadisi mazingira yao kiuhalisi na kisaikolojia. Makala hii imebaini kuwa lugha anayotumia Mai Zumo katika vichekesho teule ni ya kiudadisi. Lugha ya udadisi imejitokeza katika *Kichekesho cha Na. 1* ambapo mtoto anataka kufahamu mahusiano ya mama yake na Anko mpya. Kichekesho hiki kina wahusika watatu ambao ni Mai Zumo, Habiba Zumo (mama yake Mai Zumo) na rafiki wa mama

yake ambaye anatambulishwa kwa jina la Anko. Mama yake Mai Zumo na Anko wanaongea kuhusiana na mahusiano yao ya zamani. Mai Zumo anaingilia kati na kuanza kuwadadisi. Mai Zumo anauliza:

> **Mai Zumo**: Kwani huyu anamfahamu baba na baba anamfahamu huyu?

Udadisi huu unamfanya mama yake kubabaika huku Anko akimsukuma ili aondoke. Baada ya Mai Zumo kugundua kuwa kweli mahusiano yao ni ya siri anasema:

> **Mai Zumo**: Basi wewe endelea naye lakini mimi naenda kumwambia baba! *(Anaoneshwa akikimbia kumwambia baba yake).*

Kutokana na data hapo juu, ni wazi kuwa mhusika mtoto alikuwa anadadisi juu ya mahusiano baina ya mama yake na Anko hali ambayo hakuwai kuiona hapo mwanzo na hivyo kutamani kufahamu zaidi. Udadisi kwa watoto ni muhimu kwani huwapatia fursa ya kukua kiakili na huchochea ari ya kujifunza zaidi. Pia, udadisi huwafanya watoto waendelee kuchimbuambua na kugundua mambo ambayo baadaye huwa ni manufaa kwa jamii nzima. Katika kichekesho hiki, mtoto hamtambui Anko, wala hajui hatari itakayotokea iwapo atamwambia baba yake kuhusu huyo Anko. Kwa hiyo, kwa sababu ya mtoto kutotambua kaida za kijamii, maneno yake yanazua ucheshi kwa hadhira. Shultz (1976) anaeleza kuwa watoto wanapoonesha udadisi wao kupitia lugha, mara nyingi huvunja kanuni za kawaida za lugha au muktadha. Hata hivyo, jambo hili linakubalika kwa sababu ya uelewa mdogo wa ulimwengu wanaoanza kuujenga. Hoja hii inaonesha kuwa katika kujenga uelewa wao juu ya ulimwengu, watoto hutamani kujua zaidi juu ya mazingira yao pamoja na watu wanaowazunguka kwa kudadisi kama alivyofanya Mai Zumo katika data hapo juu.

### 4.2 Kuibua na Kutambua Hisia za Watoto

Wamitila (2003) anafafanua kuwa hisia ni muhimu kwa kuwa inasaidia kujenga dhamira. Lugha wanayotumia watoto katika vichekesho inaweza kufichua jinsi wanavyoelewa dunia na kuwasilisha hofu, matumaini na mawazo waliyonayo juu ya masuala yanayowatatiza. Makala hii imebaini kuwa lugha anayotumia Mai Zumo inaisaidia hadhira kutambua hisia za watoto. Mathalani, hadhira inaweza kuhisi uchungu, hasira, huruma, furaha au kinyaa kutokana na jinsi ilivyoipokea kazi husika. Mai Zumo katika vichekesho teule ametumia lugha ambayo inajenga hisia na hivyo kusaidia dhamira zinazowasilishwa kumganda mtazamaji au hadhira. Jambo hili linadhihirika kupitia *Kichekesho Na. 2*. Katika kichekesho hiki wazazi wa Mai Zumo wametengana, hivyo, anaishi nao kwa zamu. Baadhi ya tabia za wazazi wake zinamkera kwani haoni faraja. Hivyo, anaamua kumuelezea msaidizi wao wa kazi za ndani. Mai Zumo anasema:

**Mai Zumo:** Baba na mama siwaelewi. Nikiwa mkubwa sitaki kuwa kama wale,
sinuni kama baba wala
silewi kama mama.

Lugha ya usambamba anayotumia Mai Zumo katika data hii anaitamka kwa lafudhi ya kitoto na kuonesha jinsi ambavyo anakosa upendo wa wazazi wake. Fabb (1997) akizungumzia dhima za usambamba anafafanua kuwa usambamba unajenga hisia kwa hadhira kulingana na mpangilio wa maneno yanayodokeza wazo moja. Usambamba unaotumiwa na Mai Zumo unaonesha dhahiri kuwa hapendezwi na tabia za wazazi wake. Data iliyodondolewa inaonesha jinsi ambavyo lugha kama hii ikitumiwa na mtoto inavyojenga hisia ya huruma kwa hadhira. Kupitia Nadharia ya Uvunjaji wa Kanuni Usiokuwa na Madhara, mwasilishaji anaweza kuvunja kwa makusudi matarajio ya hadhira lakini bila kusababisha madhara. Hadhira inatambua kuwa kwa kawaida wazazi ni vielelezo bora kwa watoto (Gwako na Timammy, 2017), hivyo, watoto wanawaamini sana wazazi wao. Si matarajio ya hadhira kusikia mtoto analalamikia suala la tabia za wazazi wake hadi kufikia hatua ya kutotamani kuwa kama wao. Mhusika anatumia lugha hii kuifanya hadhira ijenge hisia ya huruma kwa mtoto kutokana na wazazi kutojali malezi ya watoto wao. Kavishe (2019) anafafanua kwamba lugha ya watoto huwa na dhima mbalimbali na miongoni mwa dhima hizo ni kuonesha wema na huruma. Hivyo, lugha ya mtoto katika vichekesho inawasaidia watazamaji kuelewa mitazamo ya watoto ambayo mara nyingi haionekani wazi, na hivyo kujenga uelewa wa kijamii na hisia za huruma kutoka kwa hadhira.

### 4.3 Kuibua Ucheshi

Lengo kuu la vichekesho ni kuchekesha (Mulokozi, 2017). Ili watu wacheke ni lazima msanii au fanani atafute mbinu mbalimbali za kuibua kicheko katika kazi yake. Ponera (2010) anasema kuwa matumizi ya lugha yana nafasi kubwa katika kuibua ucheshi. Sambamba na hilo Wanjala (2011) na Wamitila (2012) wanakubaliana kuwa vichekesho hutumia lugha na vitendo katika kuchekesha. Kwa mantiki hiyo, lugha ni msingi mkuu wa kuchekesha. Hivyo, katika vichekesho vya *Anko Zumo*, miongoni mwa dhima za lugha inayotumiwa na Mai Zumo ni kuibua ucheshi. Akijadili suala la lugha katika vichekesho, Ross (1998) anadai kuwa mtu anaweza kucheka kulingana na lugha iliyotumika kugusa hisia zake. Ross anaendelea kueleza kuwa mara nyingi vichekesho hutumia lugha ya dhihaka inayolenga kuleta utani. Hivyo, utani humfanya mtu acheke hasa ukilinganishwa na ukweli uliofumbatwa katika lugha. Kwa mfano, katika *Kichekesho Na. 4*, Mai Zumo anatoa ushauri kwa mjomba wake aliye kwenye mawazo baada ya mchumba wake kutopokea simu. Data ifuatayo inathibitisha hilo:

**Mai Zumo**: Anko, mbona umekaa kama una mawazo leo?
**Anko**: Mchumba wangu kaniacha.
**Mai Zumo**: Una gari wewe...? Pesa je? Na sura yenyewe ndo hiyo…! Umuite tu shemeji!

Data hii inaonesha ushauri anaoutoa Mai Zumo kwa mjomba wake. Kimsingi, katika jamii vijana hupeana ushauri wao kwa wao kuwa ili wawapate wanawake wazuri, sharti watafute fedha vinginevyo wataishia kuwaita shemeji. Katika kichekesho hiki, Mai Zumo anaonekana kuvunja kanuni hususani za kijamii za kutoa ushauri wa kiutu uzima kwa mjomba wake ilhali yeye (Mai Zumo) bado ni mtoto. Hadhira inaweza kucheka kutokana na uvunjaji wa kanuni usiokuwa na madhara uliotokea baada ya Mai Zumo (mtoto wa miaka minne) kutoa ushauri huu kwa mjomba wake ambaye ni mtu mzima sana akilinganishwa na umri wa Mai Zumo. Watoto mara nyingi hawafuati kanuni za kijamii. Hivyo, inapotokea Mai Zumo anavunja kanuni hizo katika uongeaji, kichekeko hutokea. Kwa kuzingatia mawazo ya Nadharia ya Uvunjaji wa Kanuni Usio na Madhara, mtoto anaweza kusema neno gumu au la kiutu uzima lakini kwa ufasaha wa kitoto. Watu wazima wanaweza kucheka kwa sababu mtoto huyo anavuka mipaka ya matarajio yao kuhusu lugha anayopaswa kutumia.

## 4.4 Kufichua Maovu

Lugha anayotumia Mai Zumo inafichua maovu yanayofanywa kwa siri katika jamii. Hoja hii inadhihirika kupitia *Kichekesho Na 7.* Katika kichekesho hiki, Mai Zumo na baba yake wanamkaribisha mgeni ambaye anatambulishwa kwa Mai kuwa ni Anko. Baada ya salamu, baba yake Mai anamuuliza mgeni juu ya kinywaji na kutoka kwenda kumfuatia maji ya kunywa. Mai Zumo anabaki na mgeni na kuanza kuongea naye. Anasema:

**Mai Zumo:** Namwambia baba mnayofanyaga na mama!

Mgeni anamsihi Mai Zumo asimwambie baba yake. Mai anaendelea kusisitiza na baada ya muda anaanza kuita:

**Mai Zumo:** Baaaba…! Baaaba…!

Data iliyodondolewa hapo juu inaonesha jinsi lugha ya mdokezo anayotumia Mai Zumo kuibua kicheko inavyotumika pia kufichua uovu. Kutokana na maelezo hayo tunaunga mkono hoja ya Mweta (2019) kuwa watoto wadogo ndio wanaweza kufichua mambo yanayofanyika sirini bila kuleta ugomvi katika jamii kwani itaonekana kuwa ni mchezo tu pamoja na kuwa ujumbe umefika. Kutokana na data hii, inaonekana kuwa kuna muktadha usiokuwa wa kawaida ambao Mai Zumo aliubaini baina ya mama yake na ‘anko’. Lugha anayotumia Mai Zumo inaonesha kwamba mama yake Mai Zumo na ‘anko’ wana mahusiano ya kimapenzi ambayo

ni ya siri. Hoja hii inadhihirishwa kupitia msisitizo unaotolewa na wananadharia ya Uvunjaji wa Kanuni Usio na Madhara kuwa suala la muktadha ni muhimu katika kuibua kicheko kwa hadhira (McGraw na Warren, 2010). Kutokana na muktadha, hadhira inatambua kuwa uhusiano wa mgeni ambaye ni ‘anko’ na mama yake Mai Zumo si mzuri kwani baba yake Mai Zumo hautambui. Hivyo, Mai kumwambia baba yake kuhusu uhusiano wa mama na ‘anko’ ni sawa na kuzua tafrani.

### 4.5 Kukuza na Kupamba Lugha

Zipo sababu mbalimbali zinazosaidia lugha kukua. Miongoni mwa sababu hizo ni kuwa na watumiaji wengi, kutumika katika shughuli za kila siku, kuibuka kwa maneno mapya na kuongezeka kwa msamiati. Katika kipengele hiki, mtafiti anaona kuwa lugha anayotumia Mai Zumo imekuwa chachu ya kukuza lugha ya Kiswahili kutokana na matumizi ya msamiati wake. Miongoni mwa msamiati huo ni ‘maguberi’. Msamiati huu unapatikana katika *Kichekesho Na. 9.* Katika kichekesho hiki, Mai Zumo anapewa simu na dada yake ili aongee na shemeji yake ilhali wote bado wanafunzi (Mai Zumo na Dada yake). Mai Zumo anapokea simu na kuanza kumkaripia shemeji yake lakini mwisho anamwambia:

> **Mai Zumo**: Lione huna hata haya, kawafuate **maguberi** huko Buguruni.

Neno lenye hati iliyokoza (**maguberi**) limetumika kumaanisha ‘malaya’ au ‘kahaba’ (TUKI, 2014). Msamiati huu si maarufu kwa watumiaji wengi wa lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo, linapotumiwa na mtoto linaleta hali ya ucheshi. Hivyo, lugha inaweza kukua na kutajirika kutokana kutumia msamiati ambao haujazoeleka. Pia, baadhi ya misimu inayotumiwa na Mai Zumo katika vichekesho mbalimbali, inasaidia kuipamba lugha ya Kiswahili na kuonekana yenye utajiri mwingi wa msamiati. Kwa mfano, ipo baadhi ya misimu ambayo imekuwa maarufu katika jamii. Misimu hiyo ni kama vile ‘pambana na hali yako’ na ‘utapata taabu sana’ katika *Kichekesho Na. 8* na ‘jeuri hiyo huna’, ‘wajumbe siyo watu wazuri’ na ‘mtaisoma namba’ katika vichekesho teule. Reuster-Jahn na Kiebling (2006) wanafafanua kuwa miongoni mwa lugha za mitaani zinazozungumzwa nchini Tanzania, misimu inachukua nafasi kubwa. Hata hivyo, wanasema kuwa lugha hii (ya misimu) huchukuliwa kama ya kihuni lakini ina mchango mkubwa katika kukuza lugha. Kwa hiyo, lugha anayotumia Mai Zumo ina mchango mkubwa katika kukuza lugha kutokana kutumia msamiati usiotumika sana ili ujulikane. Mathalani, mbali na kupamba lugha, neno ‘wajumbe’ limepanuka kimaana kulingana na matumizi yake kimuktadha. Maana hizo ni ‘wanafiki’ au ‘watu wasiokuwa na mzaha’. Upanuzi wa maana hizi unatokana na msisitizo unaotolewa na McGraw na Warren (2010). Wataalamu hawa wanasisitiza kuwa katika Nadharia ya Uvunjaji wa Kanuni Usio na Madhara,

watoto wanapovunja kanuni za kawaida za lugha, ukiukaji huo unaweza kuwa kichocheo cha kuchekesha na kuongeza uelewa zaidi wa msamiati wa lugha inayotumika. Ukiukaji wa kanuni za lugha mara nyingi unaonekana kuwa wa kuchekesha kwa sababu hadhira inatambua muktadha usio na madhara katika vichekesho. Kwa hiyo, vichekesho vimetumiwa pia kupitishia maarifa kuhusu matumizi sahihi na maana pana za msamiati na misimu.

### 4.6 Kuwasilisha Tajiriba za Watu Wazima

Wamitila (2003) anafafanua kuwa tajiriba ni dhana inayotumiwa kuelezea uzoefu wa kimaisha. Kwa hiyo, kutokana na fasili zilizotolewa hapo juu tunaweza kusema kuwa tajiriba ni uzoefu wa maisha yanayoukilia mwenendo wa mtu au jamii. Katika sehemu hii, dhana ya tajiriba itarejelea mambo yaliyozoeleka kutendwa au kuzungumzwa na watu wazima lakini yanazungumzwa na mtoto. Mfano wa mambo hayo ni masuala ya mapenzi na ndoa yanayojumuisha wivu, usaliti, limbwata, migogoro na mengineyo mengi. Mai Zumo anatumia lugha ambayo imeumbwa kisanii kufikisha tajiriba za watu wazima katika baadhi ya vichekesho teule. Ili kuthibitisha hoja hii tunajikita katika kuangalia mambo mbalimbali yanayobeba tajiriba za watu wazima katika lugha anayotumia Mai Zumo. Mambo hayo yanafafanuliwa kama ifuatavyo:

Lugha anayotumia Mai Zumo imetumika kuwasilisha masuala ya mapenzi. Kimsingi, yapo mambo katika jamii ambayo yanafahamika kuwa ama ni kwa ajili ya watu wazima au watoto. Si kitu cha kawaida kumkuta mtoto wa miaka minne akijadili masuala ya mapenzi. Kinyume chake, jambo hili limejitokeza katika vichekesho teule ambapo lugha anayotumia Mai Zumo imesheheni tajiriba za watu wazima, hususani kuhusu masuala ya mapenzi. Katika *Kichekesho Na. 5,* kwa mfano, Mai Zumo anaonekana kufuatilia kitendo cha baba yake kuongea na mwalimu faragha. Baada ya kuona wanaongea faragha anaanza kulia. Baba yake anaamua kumfuata na kuanza kuzungumza naye.

> **Baba**: Wewe, mtoto! Kwa nini unalialia?
> **Mai Zumo**: (*Anaongea huku akilia*) Mchumba wako mwalimu.

Lugha hii inaonesha dhahiri kuwa watoto wanaelewa kuwa kuna uhusiano wa kimapenzi kati ya mwanamume na mwanamke. Hivyo, wazazi wanapaswa kuacha tabia ya kujisahau na kufanya mambo yao ya kimapenzi hadharani wakidhani kuwa watoto hawafahamu. Sambamba na hayo, katika *Kichekesho Na. 9* lugha anayoitumia Mai Zumo inaonesha dhahiri kuwa inawasilisha tajiriba za watu wazima. Katika kichekesho hiki, mama yake Mai Zumo anajadiliana na mwalimu jinsi ya kukutana na baba yake Mai Zumo ili kujadili namna ya kufuatilia masomo ya binti yao. Mai Zumo anatambua ukweli kuwa mwalimu huyo ni mchepuko (nyumba ndogo) wa baba yake, hivyo anaamua kusema:

> **Mai Zumo:** Toba! Chizi kapewa rungu!

Dhihaka hii inatokana na taarifa za awali alizonazo Mai Zumo kuhusiana na mwenendo wa baba yake na mwalimu wake, hivyo, inamlenga mwalimu ambaye anajua ukweli kuwa ana uhusiano na baba yake Mai. Aidha, kauli hii inamzindua mama yake Mai Zumo na kuanza kutafakari maana yake. Kwa kutumia kauli hii ni wazi kuwa watoto wengi wanakuwa na taarifa za ziada kutokana na yale wanayoyaona au kuyasikia.

Kutokana na data hizo, inaonesha dhahiri kuwa watoto wanaposhiriki katika sanaa za maonesho, hususani vichekesho, wanatumia lugha yenye dhima anuwai kama kuwasilisha tajiriba za watu wazima. Hata hivyo, suala la watoto kushiriki katika sanaa za maonesho limewahi kutolewa maoni na wataalamu mbalimbali. Mathalani, Sifakis (1979) anaeleza kuwa si vyema kwa watoto kutumia lugha isiyoendana na umri wao kwa sababu inapoteza uhalisi wa sanaa. Tunakubaliana na hoja ya Sifakis kuwa Mai Zumo anapotumia lugha kuwasilisha tajiriba za watu wazima huifanya hadhira kutaka kufahamu iwapo lugha anayotumia mtoto anapewa au vinginevyo. Hata hivyo, tuna wasiwasi kuwa huenda lugha anayotumia Mai Zumo inaweza kumuathiri kisaikolojia. Jambo hili linajadiliwa na Saleh (2011) na Bitesigirwe (2021) kuwa lugha ya watoto inapaswa kuendana na kiwango cha saikolojia ya uelewa wake. Kwa mantiki hiyo, mtoto anapaswa kuzungumza lugha anayoielewa, vinginevyo, lugha hiyo itamuathiri katika ukuaji wake. Hata hivyo, lugha anayotumia Mai Zumo inaweza kutumika kuwasilisha tajiriba za watu wazima kutokana suala la utandawazi ambao humfanya kila mtu kujidhani kwamba ni msanii bila kujali itikeli na maadili ya sanaa katika jamii. Pia, wasanii wengine wa vichekesho hawajui kaida za kumtumia mtoto katika maigizo na athari za kisaikolojia za kumhusisha mambo ya wakubwa. Utafiti wa Wasylkiw na Currie (2011) ulibaini kuwa mhusika anaweza kubadili tabia yake kutokana na matendo anayoyaigiza pamoja na lugha anayotumia katika kuigiza. Kwa hiyo, ni muhimu kuchukua tahadhari pindi watoto wanapohitajika kutumika katika sanaa, kama vile vichekesho.

## 5.0 Hitimisho

Makala hii imechunguza dhima za lugha ya mhusika mtoto katika vichekesho teule vya Anko Zumo. Kutokana na Nadharia ya Uvunjaji wa Kanuni Usio na Madhara, makala hii imebaini kuwa lugha ya mhusika mtoto inachukuliwa kama lugha ya kitoto lakini ina dhima anuwai katika jamii. Dhima zilizobainika ni kuchochea udadisi, kuibua na kufanya hadhira itambue hisia za watoto, kuibua ucheshi, kufichua uovu, kukuza na kupamba lugha na kuwasilisha tajiriba za watu wazima. Sambamba na hayo, imebainika kuwa watoto wanapotumia lugha hasa kuwasilisha tajiriba za watu wazima kuna hatari ya maudhui hayo kuacha athari hasi katika mwenendo wa tabia yake na ukuaji. Kutokana na hayo, makala hii inatoa wito kwa watunzi wa sanaa zinazohusisha watoto kuwa ni muhimu kuzingatia saikolojia ya watoto katika kuwapatia maudhui wanayopaswa kuwasilisha.

## Marejeleo

Bisht, R. (2008). "Who is a Child? The Adults Perspective Within Adults-Child Relationship in India". *Interpersona*. 2(2):151-172.

Bitesigirwe, T. (2021). Dhima ya Lugha Anayotumia Mhusika Mtoto Katika Vichekesho teule vya *Anko Zumo*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Bruner, J.S. (1983). *Child's Talk: Learning to Use Language*. Oxford: Oxford University Press.

Currie, M. na Wasylkiw, L. (2011). "Animal House Effect: How University -Themed Films Affect Students Attitudes". *Psychology Education.* 15: 25-45.

Ernest, J. (2020). "Yuko Wapi?" *Bingwa*, Februari 18, uk. 12.

Gwako, B. na Timammy, R. (2017). "Uchanganuzi Linganishi wa Suala la Maadili kwa Vijana wa Kiume katika Tenzi Mbili za *'Siraji'* na *'Adili'". Mwanga wa Lugha*. 2(1): 134-148.

Fabb, N. (1997). *Linguistic and Literature: Language in Verbal Arts of the World*. Brackwell: Oxford.

Kavishe, A.R. (2019). Ujitokezaji wa Falsafa ya Ubuntu katika Riwaya ya Kiswahili: Uchunguzi wa *Adili na Nduguze* (1952) na *Siku ya Watenzi Wote* (1968). Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mcgraw, A.P. na Warren**, C.** (2010). Benign Violations Making Immoral Behavior Funny. *Psychological Science.* 21(8):1141-1149.

McGraw, P.A. na Wolff, J. (2012). "The Benign Violation Theory: A Functional Account of Humor". *The Oxford Handbook of Humor Research*. 11:24-37.

Mulokozi, M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*: *Kozi za Fasihi Vyuoni na Vyuo Vikuu*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Mweta, E. (2019). Matumizi ya Nyimbo za Watoto katika Muziki wa Bongo Fleva. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Ngugi, P.M.Y. (2014). "Fasihi ya Watoto katika Kutekeleza Mahitaji ya Kisaikolojia ya Mtoto." *Kiswahili.* 77: 170-180.

Ngugi, P.M.Y. (2018). "Nafasi ya Ubunifu katika Mchezo wa Watoto *Michongoano*." *Kioo cha Lugha*. 67- 69.

Olajimbiti, E. (2018). "Discourse Represantation of Nigerian Children's Experiences and Humour in Selected Comedy of Emmanuella". *Red Feather* (9) 2: 1-18.

Orellana, S. (2017) *A Childish Theory of Comedy: On the Childish Origins of Humor and How the Humor of Children Can Help Us Become Naturally Funnier Subjects*. Independently Published

Piaget, J. (1954). *The Construction of Reality in the Child*. New York: Basic Books.

Ponera, A.S. (2010). Ufutuhi Katika Nathari za Shabaan Robert: Maana yake, Sababu za Kutumiwa na Athari zake kwa Wasomaji. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Reuster-Jan, U. na Kiebling, R. (2006). "Lugha ya Mitaani in Tanzania: The Poetics

and Sociology of Young Urban Style of Speaking,With a Dictionary Comprising 100 Words and Phrases." *Swahili Forum.* 13: 13- 14.

Ross, A. (1998). *The Language of Humor*. New York: Routledge.

Samwel, M. (2013). *Tamthiliya ya Kiswahili: Kutoka Miviga ya Kidini Hadi Filamu*. Dar es Salaam: MEVELI.

Mwakisyala, M. (2020). Uchunguzi wa Mbinu za Kiutendaji katika Vichekesho Teule vya *Ze Orijino Komedi*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Senkoro, F.E.M.K. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Sifakis, M. (1979). "Children in Greek Tragedy". *Bulletin of the Institute of Classical Studies.* 26: 1-15.

Shultz, T.R. (1976). A Cognitive-developmental Analysis of Humor. Katika Chapman A. H. na Foot, C. H (Wah.), *Humour and Laughter: Theory, Research and Application* London: Wiley. Kur. 11-36.

TUKI (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la Tatu). Dar es Salaam: TUKI.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Limited.

Wamitila, K.W. (2012). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi.* Nairobi: Focus Publication Limited.

Wanjala, F.S. (2011). *Kitovu cha Fasihi Simulizi kwa Shule, Vyuo na Ndaki*. Mwanza: Serengeti Bookshop Pulishers.

Wilkie, I. na Saxton, M. (2010) "The Origins of Comic Performance in Adult-Child Interaction *Comedy Studies*, 1: 21-32.

**Diskografia**

Anko Zumo. (2018). Kutoka https://www.youtube.com/watch?v=Z7eXDP5QAzw Imetazamwa tarehe 18/9/2020.

Anko Zumo. (2018). Kutoka *https://www.youtube.com/watch?v=VQe0O05tyUw.* Imetazamwa Tar. 20/7/2021.

Anko Zumo. (2018). https://www.youtube.com/watch?v=8hFh5dLzLII Imetazamwa tar. 12/7/2021.

Anko Zumo (2018). Kutoka https://www.youtube.com/watch?v=Z97ZDdueE5w Imetazamwa tar. 12/9/2021.

Anko Zumo. (2018). Kutoka https://www.youtube.com/watch?v=Z97ZDdueE5w Imetazamwa tar. 18/9/ 2021.

Anko Zumo (2018). Kutoka https://www.youtube.com/watch?v=1CVYIv1bsfA Imetazamwa tarehe 12/3/2021.